



# EP EBOOKS

This document is tracked, do not share

# MALENGA WA KENYA

***(Kwa Gredi 1, 2 & 3 - Mtaala mpya wa umilisi)***


## Wahariri

**Timothy Omusikoyo Sumba**
**Kaka Fred**
**Tabitha Mawia Manzi**

HAKIMILIKI ©2021 NA **KakaFred**

**Haki zote zimehifadhiwa**

Haki zote zimehifadhiwa. Nimarufuku na hatia kwa wenye silica za kugushi, kuiga, kubadili, kuchapisha, kutafsiri, kuigiza au kutumia mbinu zozote bila idhini ya mwandishi kupitia kwa wakili kulingana na (*Copyright, Design and Patents Act)* ya 1988.

Mtu yeyote atakayefanya kitendo chochote kinyume na sheria anaweza kushtakiwa.

Toleo la kwanza: Machi 2020

Kimechapishwa na Elong'o Publishers

P.O BOX 944, Narok

Baruapepe: info@elongopublishers.co.ke

Rununu: +254742433826

**ISBN: 9798728306368**

## DIBAJI

Malenga wa Kenya ni diwani ya ushairi kwa hadhira lengwa ya shule za msingi hususan wanafunzi wa gredi za kwanza hadi tatu. Tungo za kisasa zinazoukumbatia mtaala mpya wa elimu - umilisi, zimetawala. Mada kuu zimedondolewa silabasini ili kutungiwa mashairi mwafaka. Isitoshe, msamiati tangulizi ni ule sahili uliooneshwa silabasini ili mwanafunzi aanzie kwa ajuayo kabla ya kukabiliana na wastani kisha mengineyo ya kumfikirisha zaidi. Mashairi mengi yaliyosheheni ubunifu yanasisimua hadi ya kusisimua. Kimsingi, azma ya washairi ni kuelimisha kwa ucheshi, burudani na kimchezo. Utafiti waonyesha kuwa kusoma kwa aina hii hakuchoshi akili. Pia maswali ya kujitathmini uelewa kulingana na malengo ya mtaala wa umilisi.

Ushairi ni nguzo kuu katika fasihi ya watoto wenye kiu ya kujua na Kufahamu mzo wa mambo. Matumaini yetu ni kuwa kwa kusomasoma na kughanighani mashairi aina ya tathnia, tathlitha, tarbia, takhmisa, tasdisa ngonjera na guni wanafunzi watajichotea ubunifu utakaowafanya kuwa malenga, manju na waghani wa kupigiwa mifano mnamo siku za usoni. Kila la heri katika usomaji na ughani wenu.

**Timothy Omusikoyo Sumba,**
**Mwandishi, mwalimu mshauri na mhariri wa kazi bunilizi.**

# YALIYOMO

DIBAJI......iv

KALAMU YANGU ...... 8

LIPENI KARO NISOME ......10

TAA ZA BARABARANI ......12

NAKUPENDA  KENYA ......14

MIEZI YA MWAKA ......16

LISHE BORA ......18

AKISAMI ......21

SIKU ZA WIKI ......24

MIMI ......26

NG'OMBE WANGU ......28

PAKA WANGU ......30

HAKI ZANGU......32

KAZI MBALIMBALI ......34

SHULENI ......37

NIKO SALAMA ......39

SAFARI YANGU ......41

MIEZI NA SHEREHE ZA UMMA ........................................ 43

ANAYEIPENDA NCHI ........................................ 45

NIDHAMU MEZANI ........................................ 47

UZALENDO ........................................ 50

NITAJIJUA ........................................ 52

SALAMU ........................................ 54

TULENI VYAKULA BORA ........................................ 56

MIEZI ........................................ 58

PAKA WANGU ........................................ 60

KAZI ZETU ........................................ 62

NAOMBA HAKI ........................................ 64

VYAKULA VYA MADHARA ........................................ 66

VYAKULA BORA ........................................ 69

VYAKULA HATARI ........................................ 72

KARIBU DARASANI ........................................ 74

MIEZI YA MWAKA ........................................ 76

NG'OMBE WETU ........................................ 78

HAKI ZETU ........................................ 80

SIKU YA SOKO ........................................ 82

**USAFI WA MWILI** ........................................................................................ **84**

**FAMILIA YETU** ........................................................................................ **86**

**KAZI MBALIMBALI** ........................................................................................ **88**

**KORONA LITOKA WAPI?** ........................................................................................ **90**

**VIKEMBE** ........................................................................................ **92**

**MAMA YANGU** ........................................................................................ **95**

**USAFI** ........................................................................................ **97**

**MAPISHI** ........................................................................................ **99**

**HAKI YANGU** ........................................................................................ **101**

**KAZI** ........................................................................................ **103**

**VYAKULA BORA** ........................................................................................ **105**

**USAFI WA MAZINGIRA** ........................................................................................ **106**

**KALAMU IMEPOTEA** ........................................................................................ **107**

**MWALIMU** ........................................................................................ **109**

## KALAMU YANGU

**Mtunzi: Kaka Fred**
**Lakabu: Malenga Dhahabu**
**Gatuzi: Trans Nzoia, Kenya.**

Kalamu niipendayo, ni hii nayotumia,
Hati niandikayo, huwa nzuri mara mia,
Marafiki kina Piyo, wao huitamania,
Kalamu yangu asante, kwa kunipa hati bora,

Mwalimu Piu ajapo, hupongeza hati yangu,
Pipi humumunya hapo, ikiwa zawadi kwangu,
Niendapo huwa ipo, haikosi Shanta yangu,
Kalamu yangu asante, kwa kunipa hati bora,

Nahidi nitaitunza, isije ikaibiwa,
Mwandiko nitautunza, kila mara kusifiwa,
Kalamu imenifunza, uzuri kuzawadiwa,
Kalamu yangu asante, kwa kunipa hati bora,

**Jitathmini**

1. Je, Unakumbuka shairi?
2. Mbona ninapenda kalamu yangu?
3. Mbona hati ya yangu huwaa nzuri?

4. Mwalimu Piu hunipa nini aingiapo darasani?
5. Je, wewe unaipenda kalamu yako?
6. Kwa nini unastahili kuitunza kalamu yako?

## LIPENI KARO NISOME

**Mtunzi: Kaka Fred**
**Lakabu: Malenga Dhahabu**
**Gatuzi: Trans Nzoia, Kenya.**

Walezi wangu sikia, nimechoka kuumia,
La moyoni nawambia, sitaki kushika njia,
Nisikilize wazazi, lipeni karo nisome,

Kila niwapo shuleni, waalimu wanisema,
Mara silipi mapeni, deni langu ni mlima,
Nisikilizeni wazazi, lipeni karo nisome,

Mjarabu sikufanya, muhula uliopita,
Takataka nilisanya, ndio muda ukapita,
Nisikilizeni wazazi, lipeni karo nisome,

Nijapo kule nyumbani, hunipi karo yenyewe,
Badala yake shambani, nikalime kwa wenyewe,
Nisikilizeni wazazi, lipeni karo nisome,

Taaluma ya angani, sitaki niipoteze,

Kubali kuwa mdeni, nitalipa nikisoma,

Urubani una mapeni, nitasimama kwa wima,
Nisikilizeni wazazi, lipeni karo nisome,

**Jitathmini**

1. Mbona mwandishi hataki kufukuzwa shuleni?
2. Taja umuhimu wa kuenda shuleni.
3. Ukimaliza shule ungependa kuwa nani?
4. Urubani no kazi gani?
5. Shairi hili Lina beti ngapu?

## TAA ZA BARABARANI

**Mtunzi: Lilian Alividza**
**Lakabu: Malkia wa Nyikani**
**Gatuzi: Kakamega, Kenya.**

Na taa za kuongoza, magari huwa ni tatu,
Polepole nakujuza, waziwazi kila kitu,
Ni hatia kupuuza, kupuuza sithubutu,
Taa za barabarani, hutoa maelekezo.

Rangi nyekundu jamani, huelekeza si siri,
Dereva awe makini, akasimamishe gari,
Asijiweke tabani, kwa kukaidi amri,
Taa za barabarani, hutoa maelekezo.

Na rangi ya kaharabu, dereva awe tayari,
Kuondoka kwa adabu, kwendelea na safari,
Dereva ana wajibu, yalo mema kufikiri,
Taa za barabarani, hutoa maelekezo.

Kuna rangi ya kijani, ni muhimu kwa hakika,
Mtembeaji njiani, anastahili kuvuka,
Tena vuka kwa makini, haraka hina baraka,
Taa za barabarani, hutoa maelekezo.

**Jitathmini**

1. Taa za barabarani zina umuhimu upi?
2. Taa ya rangi ya kijani kibichi mtembeaji anapoiona anahitajika kufanya nini?
3. Dereva anapoiona taa ya rangi ya kaharabu anaitajika kufanya nini?
4. Taja rangi tatu za taa za barabarani?

## NAKUPENDA KENYA

**Mtunzi: Lilian Alividza**
**Lakabu: Malkia wa Nyikani**
**Gatuzi: Kakamega, Kenya.**

Nchi yangu ni Kenya, mzalendo namba wani,
Yalo mema ninafanya, kenya ninakuthamini,
Tuilinde yetu Kenya, nchi yetu sio duni,
Kenya wapendeza sana, daima nitakupenda.

Mandhari ya kuvutia, mbuga zetu nzuri sana,
Kenya sana wavutia, Kenya wewe ni mngwana,
Siwezi kukuchukia, nakupenda tena sana,
Kenya wapendeza sana, daima nitakupenda.

Kenya ndiye baba yangu, vilevile ndiye mama,
Wakujua ulimwengu, weye hupendi zahama,
Akakubariki Mungu, uwe nchi ya heshima,
Kenya wapendeza sana, daima nitakupenda.

Unang'aa na kung'aa, Kenya unameremeta,
Waangaza kama taa, kamwe hupendi matata,
Wewe acha kuzubaa, tuishi bila ya utata,
Kenya wapendeza sana, daima nitakupenda.

**Jitathmini**

1. Jina mzalendo lina maana ipi?
2. Taja kichwa cha shairi hili?
3. Kenya ndiye baba yangu, vilevile ndiye-----------?
4. Kenya ina mandhari gani?

## MIEZI YA MWAKA

**Mtunzi: Elisha Otoyi (Isah Bin Omar)**
**Lakabu: Malenga wa Wanyonge**
**Gatuzi: Homabay, Kenya.**

Katika mwaka mmoja, tunayo miezi kumi na miwili,
Shughuli zao ni tofauti, kuanzia mwanzo hadi mwisho.

Wa kuanza ni Januari, mashamba yanatayarishwa,
Wazazi wanafyeka, na kutoa uchafu ndani.

Kisha tunayo Februari, mwezi huu ni wa pili,
Tunashirikiana kulima, tukisubiri mvua.

Halafu wa tatu ni Machi,  mwanzo wa mvua kunyesha,
Mimea inapata maji, na kukua kwa urefu.

Ukifika Aprili, maji ni mengi shambani,
Kupalilia tunarauka, ili mihindi na miharage ipata kukua vyema.

Ule wa tano ni Mei, kupalilia twarudia,
Ile tuweze kufurahia, mavuno tele.

Juni na hata Julai, kazi za shamba zinapungua,

Mvua ni rasharasha tu, dawa twanyunyizia mimea.

Shangwe na vigelegele, ni mwezi wa Agosti,
mavuno ya jasho letu, yatiwa ndani ya gala.

Septemba na Novemba, wazazi huuzia shule mavuno,
Ili kugharimia karo yangu, niendelee kusoma.

Mwisho wa mwaka ni Disemba, Shamba letu hutayarishwa tena,
Krismasi twasherehekea, kwa pesa za kutoka shambani.

Miezi hiyo ikiisha, hukaribisha mwaka mpya,
Usisahau rafiki yangu, kwa jumla ni kumi na miwili.

**JITATHMINI**

1. Taja miezi yote ya mwaka
2. Kazi gani hufanyw katika mwezi wa Januari?
2. Ni mwezi gani watu hushirikiana kulima?
3. Watu husherehekea Krismasi katika mwezi upi?
4. Wazazi wanauza mbegu za mimea gani mnamo Septemba na Novemba?
5. Kazi za shamba hupungua katika miezi gani?

## LISHE BORA

**Mtunzi: Elisha Otoyi (Isah Bin Omar)**
**Lakabu: Malenga wa Wanyonge**
**Gatuzi: Homabay, Kenya.**

**Mwalimu**
Sabalkheri wanafunzi, naomba mkaketi,
Kipindi cha leo, ni kuhusu afya zetu,
Vyakula vipi mwavipenda, mkivila mna raha,
Kila mmoja yuko huru, ukweli na tukaseme.

**Wanafunzi**
Akheri mwalimu mpendwa, twashukuru kwa nafasi hii,
Kwa kawaida sisi hula, vyakula vifuatavyo,
Vitamini twatambua, protini na hata wanga,
Kwa hivyo twaomba kujua, iwapo ulimaanisha hivi au vipi?

**Mwalimu**
Jibu lenu nalipenda, asanteni kuchangamka,
Hata hivyo sijatosheka, nilitaka mvitaje,
Kwa orodha nikajue, mifano ya vyakula hivyo,
Masikio yangu nimeyatega, mpira nawarushia.

**Wanafunzi**
Tumekupata kabisa, swali mboga umetuuliza,
Sukari biskuti na peremende, vyote hutupa nguvu,
Keki soda hata juisi, tuna sababu za kuvipenda,
Hutupa nguvu hakika, kuanzia asubuhi hadi Jioni.

**Mwalimu**
Hivyo basi mlivyotaja, mwavila kila siku?
Au mnavyo vingine, vya kuongezea orodha yenu,
Niambieni nifunzike, elimu ni ya watu wote.
Kwa jina moja vyaitwaje, niweze kuelewa.

**Wanafunzi**
Darasani utakuwa, ukapate elimu bure,
Kwa jumla ita wanga, ukipenda kabohaidreti,
Vingine hatujasahau, sharubati na hata chipsi,
Chokoleti na soda ya Vanta, tumechanuka Bwana Afya.

**Mwalimu**
Naona muda walekea kwisha, kuhusu kipindi hiki,
Haraka haraka tajeni, vya protini na vitamini,
Michango yenu nafurahia, nitakuwa mwalimu tukimaliza,
Protini na vitamini, msirudi kwa wanga.

**Wanafunzi**

Kwa kuwa chipsi ni tamu, yafaa kuwa protini,
Tukishaikula, kwa uma twanenepa,
Miilini twajengeka, kunenepa kama ngurue,
Vitamini ni sharubati, ukiipata nayo keki.

**Mwalimu**

Asanteni kusema ukweli, unaotoka mioyoni mwenu,
Napenda kuwaonya kuhusu mliyotaja,
Japo ni vyakula vyetu, vinadhuru zetu afya,
Daftari lako basi chukua, upate mwanga wangu.

Vyakula vyenye wanga, kuleni ninavotaja,
Asali wali na chapati, uji wa mtama au wowote,
Epukeni mlivosema, huharibu meno na kinga ya mwili,
Tumieni maziwa na mayai, nyama nyeupe na samaki.

**Wanafunzi**

Na sasa vikiwa hivi, vitamini tuwe na gani,
Juzi kiranja kaenda hospitali,kapatikana na saratani,
Swali letu ni hili, kwa nini kapata ugonjwa,
Sote tulihuzunika, kwani hatukutarajia huo.

**Mwalimu**

Ninapomaliza somo, ningependa kuwambia,

Vitamini si chakula ghali, ni rahisi na cha kawaida,
Tumia mboga zote, matunda uyaongeze,
Magonjwa tutazuia, tutaishi kwa miaka mingi.

**Mwalimu**
Swali hilo mnalouliza,jibu lake nyote mnalo,
Someni vitabu vya Sayansi, ambavyo nimewapatia,
Mtajua chanzo chao, na vyakula twafaa kula,
Muda wangu umekwisha, kwaherini kwa sasa.

**Wanafunzi**
Mawaidha tumepata, hongera bwana Afya,
Tabia zetu tubadili, kuhusu tunachokula,
Tusiseme ni vitamu, tufikirie madhara yao.
Kauli moja tunasema, afya yetu ni muhimu.

**JITATHMINI**

1. Jibu la salamu sabalkheri ni nini?
2. Taja aina tatu za vyakula
3. Ni vyakula gani vinavyoleta madhara mwilini?
4. Taja vyakula viwili vya
    a. Wang
    b. Vitamini
    c. protini
5. Mwalimu anaitwaje katika shairi hili?

## AKISAMI

**Mtunzi: Okwalo Wambani**
**Lakabu: Malenga wa Mitume**
**Gatuzi: Busia, Kenya.**

1 moja sahani nzima,
1/2 mbili nusu ya sima,
1/3 tatu thuluthi nafuma,
1/4 nne robo napima.

1/5 tano nauma humusi,
1/6 sita mebaki sudusi,
1/7 saba subui kiasi
1/8 nane thumni kiasi.

1/9 Tisa tusui napata,
1/10 kumi ushuri kamata,
Kizima sasa mekata,
Akisami sina utata.

**Jitathmini**

1. Ukigawa sahani ya sima mara mbili sawa utapata……
¼ huitwa …………….
2. Akisami ya mwisho hapa ni ipi?

3.  Ukiwa na tunda moja na ugawe mara tisa utapata akisami gani?

4. Akisami 1/3 huitwa ……….

## SIKU ZA WIKI

**Mtunzi: Okwalo Wambani**
**Lakabu: Malenga wa Mitume**
**Gatuzi: Busia, Kenya.**

Ni Sabato Jumamosi, siku ya kwanza ya wiki,
Jumapili sina mkosi, kanisani kushiriki,
Asante mwenyezi Mungu, wiki nzuri kutuundia.

Jumatatu mimi Tatu, shuleni naelekea,
Jumanne si mtukutu, mawaidha nafuatilia,
Asante mwenyezi Mungu, wiki nzuri kutuandalia.

Jumatano ya tano ndiyo, usafi wa shuleni,
Sisahau Alhamisi, Kiswahili kukiongea,
Asante Mwenyezi Mungu, wiki nzuri kutuundia.

Ijumaa nayo najua, wiki mimi nafungia,
Msikiti takimbilia, dua zangu kutolea,
Asante mwenyezi Mungu, wiki njema kutuundia.

**Jitathmini**

1. Ni siku gani ambayo mwandishi huenda msikitini?
2. Siku ya kwanza ya wiki ni ………. ilhali siku ya mwisho ni ……..
3. Siku ya Jumapili mwandishi huenda……….

4. Siku ipi na ipi ambyo bendera hupandishwa shuleni kwenu?
5. Siku ya katikati ya wiki ni .... nayo ya tano ni ......
6. Jina lingine la wiki ni ........

## MIMI

**Mtunzi: Alfred Lobawoi**
**Lakabu: Mweledi Chipukizi**
**Gatuzi: Turkana, Kenya.**

Jina kamili ni Ali, wengi ndivyo wanijua,
Ni mdogo wangu mwili, kama jitu sijakua,
Napenda kucheza boli, pia geli ninajua,
Mimi ni Ali.

Nasomea baharini, shule yetu ya msingi,
Gredi ya kwanza ndani, lenye wanafunzi wengi,
Darasa langu kusini, lenye uwekundu rangi,
Mimi ni Ali.

Umri ni myaka saba, mfupi tena wa kimo,
Nimemfuata Baba, ni kama mimi kwa kimo,
Oli huniita miba, kwa sababu tu ya kimo,
Mimi ni Ali.

Kijiji changu kwa kweli, huitwa Mwembe tayari,
huwa twapenda kusali, kwa kila Alfajiri,
Sitoongeza asali, wakati wangu nakiri,
Mimi ni Ali.

**Jitathmini**

1. Ali anasomea shule gani?
2. Ali ana miaka mingapi?
3. Kijiji cha kina ali kinaitwaje?
4. Ni mchezo upi ambayo Ali anapenda?
5. Rafiki wa Ali anaitwaje?

## NG'OMBE WANGU

**Mtunzi: Alfred Lobawoi**
**Lakabu: Mweledi Chipukizi**
**Kaunti: Turkana**

Mnyama nimpendaye, wangu mimi ndiye ng'ombe,
Nampenda sana yeye, nimuonapo na pembe,
Yeyote kando na yeye, simuoni ndiye tembe.

Napenda sana maziwa, meupe pepepe! tena,
Hayo ni tamu ja muwa, na hata sitapeana,
Mimi humpa mauwa, mpendwa wangu Kimwana.

Yeye hunipea ngozi, ya kutengeneza vitu,
Kama ilivyo tu jozi, hizo hizo za viatu,
Tena hunipea kazi, na kujuana na watu.

Nyama yake ni mtamu, nikila kwenye sahani,
Ninapotia saumu, pamoja na biriani,
Sisahau yake damu, mimi hunywa niamini.

Kila akila chakula, huniita langu jina,
Moo! Hata nikilala, mimi husikia sana,
Huwa tunasali sala, kumuomba Maulana.

Anapenda kula nyasi, pamoja na kunywa maji,
Hataki hata juisi, hata nikimpa uji,
Hata sina wasiwasi, afya bora huhitaji.

**Jitathmini**

1. Makao ya mnyama anayezungumziwa huitwaje?
2. Eleza faida za ng'ombe.
3. Rangi ya maziwa ni gani?
4. Taja Wanyama wengine wa nyumbani unaowajua.
5. Ubeti wa mwisho una mishororo mingapi?
6. Eleza namna ng'ombe anavyotunzwa.

## PAKA WANGU

**Mtunzi: Alfred Lobawoi**
**Lakabu: Mweledi Chipukizi**
**Gatuzi: Turkana, Kenya.**

Nampenda paka wangu, jina lake ni kipusi,
Hukaa karibu yangu, pia hata kula nasi.

Nyeupe ndo rangi yake, na hana madoadoa,
Ninapenda sura yake, mtulivu wa kupoa.

Mimi humpa maziwa, nyau! Akinililia,
Sahanini anajuwa, nyama nimemkatia.

Anapenda kukimbia, anaponiona mimi,
Ishara kufurahia, kwamba anipenda mimi.

Mimi tena humlinda, asije akaumizwa,
Siku zote nampenda, sitaki aje kuuzwa.

**Jitathmini**

1. Ni mnyama yupi anayetajwa katika shairi hili?
2. Chakula cha paka ni maziwa na nini?
3. Paka huyo alikuwa na rangi aina gani?

4. Jina la paka huyo ni nani?

## HAKI ZANGU

**Mtunzi: Patrick Kioko**
**Lakabu: Mwana Kidagala**
**Gatuzi: Machakos, Kenya.**

Shika moja nikwambie, najua haki zangu,
Moja elimu nipatie, niondoe uzuzu wangu,
Kusoma moja na mbilie, niupasi mtihani wangu,
Haki zangu, haki zangu.

Shika mbili nilonge, haki yangu lishe bora,
Tumetetewa kwa bunge, watoto tupate ilio bora,
Miili isiwe nyonge, kama simba tuwe imara,
Haki zangu, haki zangu.

Shika taatu niambe, ngine kupewa malezi,
Mama baba tuma jumbe, makinda wapewe malezi,
Kukosa ili uhambe, kutukanisha ulezi,
Haki zangu, haki zangu.

Shika nne nikuli,bleo nasema bayana,
Mavazi mema amali, haki yangu mie mwana,
Kufikishwa hospitali, naugua na nina,
Haki zangu, haki zangu.

Haki yangu mwana, kucheza ko uwanjani,
Kucheka furahi sana, kuongeza siku usoni,
Kupendwa na baba nina, tanitia raha moyoni,
Haki zangu, haki zangu.

Kalamu yangu mekwama, wino ndoo umekwisha,
Lau sana ningesema, haki nyingi zijakwisha,
Imara Kama chuma, haki za watoto dumisha,
Haki zangu, haki zangu

## KAZI MBALIMBALI

**Mtunzi: Jimmy Kiplimo Naibei**
**Lakabu: Malenga Jimmy wa Jimmy**
**Gatuzi: Bungoma, Kenya.**

Waache wana wasome ,matabibu wao wawe,
Msiwafanye wakalime, waalimu waajiriwe,
Ndege pia ingurume, marubani wao wawe,
Duniani kuna kazi, funguo zake ni elimu..

Waalimu mashuleni, makasisi kanisani,
Wausaji madukani, taniboi barabarani,
Mkwezi yu mnasini, halimali wa mkokoteni,
Duniani kuna kazi, funguo zake ni elimu.

Wapo wengi ni kinyozi, nywele wao kuyakata,
Wasusi tele kinyozi, nywele wao kusokota,
Yuko pia mfinyanzi, bora vyombo tunapata,
Duniani kuna kazi, funguo zake ni elimu.

Wapo tele wahunzi, vyuma wao kufanya,
Soma uwe mpishi, pishi mlo kuufanya,
Utingo ni bora kanzi, yatubidi kuufanya,
Duniani kuna kazi, funguo zake ni elimu.

Duniani kuna kesi, jemedari ni wakili,
Unajimu pia kazi, kuwa bore sikubali,
Urinaji pia kazi, shughulika na hasali,
Duniani kuna kazi, funguo zake ni elimu.

Shule yetu ni nzuri, heko bawabu wetu,
Madereva ni wazuri, watubeba toka kwetu,
Michezoni mwa refari, usalama bora kwetu,
Duniani kuna kazi, funguo zake ni elimu.

Mashairi tamutamu, malenga manju kayatunga,
Wausaji wakarimu, meneno matamu wamepanga,
Waazigi wakarimu, mifupa mwili tayapanga,
Duniani Kuna kazi, funguo zake ni elimu.

**Jiitathmini.**

1. Shairi hili ni la beti ngapi?
2...ni baada ya kupata.......ndipo utapata kazi
3. Ubeti wa mwisho una mishororo mingapi?
4. Madereva wanatusaidiaje?
5. Eleza watu hawa hufanya kazi gani?
    a) mhazigi
    b) mhuguzi
    c) refa

d) mwalimu

e) hamali

6. Je, ungependa kufanya kazi gani ukubwani? Kwa nini?

## SHULENI

**Mtunzi: Bright Odeng**
**Lakabu: Nuru Gizani**
**Gatuzi: Siaya, Kenya.**

Ninafika kwa shule, kengele inapigwa,
Tunaenda kwa gwaride, bendera inapandishwa,
Walimu wanatoka kwa ofisi, na kuongea na sisi,
Tunarudi darasani, na masomo kuanza.

Ninaketi kwa dawati, natoa kitabu na daftari,
Kichongeo nachongea kalamu, kisha nakiweka kwa seti,
Mwalimu anaandika, kwa ubao akitumia chaki,
Tunasoma somo la kwanza, kisha linakamilika.

Somo jingine tena, mwalimu anaingia,
Anafuta ubao, akitumia kifutio ama dasta,
Napiga mstari kwa kitabu, nikitumia rula,
Nafuta mandishi maovu, nikutumia raba.

Tunakusanya madaftari, na kuvipea mwalimu,
Na tunaingia kwa maktaba, na kusoma vitabu vya hadithi,
Saa kumi inapofika, begi yangu mgongoni,
Naingia kwa gari ya shule,ninarudi nyumbani.

**Jitathmini**

1. Mwalimu anatumia nini kufuta ubao?
2. Wanafunzi wanasoma vitabu vya hadithi wapi?
3. Walimu wote huketi wapi wanapokuwa shuleni?
4. Bendera hupandishwa wanafunzi wanapokuwa wamesimama wapi?
5. Tunatumia nini kupiga mstari kwa daftari?

## NIKO SALAMA

**Mtunzi: Vincent Imbali.**
**Lakabu: malenga mwona mbali**
**Gatuzi: Vihiga, Kenya.**

Usalama ni muhimu, popote unapokuwa,
Kwetu si binadamu, ni muhimu ukijuwa,
Ninaomba uje humu, usalama kuujuwa,
Nitakuwa imara, kulinda usalama Wangu.

Sichezei kwa mvua, nisije nikaugua,
Nako uwanjani pia, sitotaka kujikwaa,
Mashimo taangalia, sitaki kutumbukia,
Nitakuwa imara, kulinda usalama Wangu.

Nikiwa barabarani, hakika sitakuchezea,
Tatembea kwa makini, nikiwa nimetulia,
Na maji sitachezea, ninaweza kuzamia,
Nitakuwa imara, kulinda usalama wangu.

Mizinga nayo hatari, kamwe sitaichezea,
Nyuki wauma si siri, hili mimi najua,
Visima pia hatari, naweza kutumbukia,
Nitakuwa imara, kulinda usalama Wangu.

**Jitathmini**

1. Jaza mapengo.
    a) us_l_m_
    b) m_k_n_
    c) _i_im_
2. Ukichezea karibu na mashimo unaweza?__________
3. Kwa nini si vizuri kuchezea mizinga ya nyuki?

## SAFARI YANGU

**Mtunzi : Vincent Imbali**
**Lakabu: malenga mwona mbali**
**Gatuzi: Vihiga, Kenya.**

Nikitaka kwenda mbali, mimi hupanda matwana.
Kisha nalipa nauli, pasipo na kubishana.

Taniboi hunipakia, mizigo kwa keria.
Kisha sisi abiria, garini tunaingia.

Steji yangu nikifika, hapo Mimi hushukia.
Bodaboda hutumika, nyumbani kusafiria.

Mizigo ikiwa mingi, garimoshi ndilo sawa.
Mabehewa yake mengi, ya mizigo kubebewa.

Siku nitaenda ng'ambo, nitapanda eropleni.
Rubani afanye mambo, nifurahi safarini.

Nikirudi nipande meli, nisafiri baharini.
Kisha nahodha wa meli, aniweke bandarini.

Nikifika bandarini, nitapanda farasi.

Ama ni'ngie basini, ili nifike kwa kasi.

**Jitathmini**

1. Mimi huchukua nauli kwenye matwana. Naitwa nani?
2. Eropleni husafiria wapi?
3. Wasafiri wa garini pia huitwa?
4. Nani huongoza mel
5. Je, taniboi ni nani?

## MIEZI NA SHEREHE ZA UMMA

**Mtunzi : Ali M. Mwanza**
**Lakabu: Malenga Kande**
**Gatuzi: Kwale, Kenya.**

Ifikapo Mei mosi, siku ya wafanyakazi,
Twasherehekea sisi, siku ya wafanyakazi,
Wanaookoa sisi, kwa mengi tele malezi,
Ni halali kwa katiba, siku ya wafanyakazi.

Juni hufika haraka, wakenya mwezi muhimu,
Kufurahi madaraka, yaliyo kwetu muhimu,
Wakoloni tulopoka, wongozi ulo muhimu,
Juni mosi ikifika, Madaraka kenya yetu.

Oktoba tunapaa, siku iliyo halua,
Kutambua mashujaa, kushinda walosumbua,
Ni siku inayofaa, sisi sote kuijua,
Ishirini Oktoba, kila mwaka mashujaa.

Desemba ni mashuhuri, kwa zima taifa letu,
Kufurahi jamhuri, kumiliki nchi yetu,
Kwa kuwa tulisubiri, kupewa kibali chetu,
Desemba kumi na mbili, ni siju ya Jamhuri.

Jitathmini

1. Tarehe ishirini Oktoba tunasherehekea siku kuu ya __________________________ kila mwaka nchini Kenya.

2. Kwa nini ni muhimu kusherehekea siku kuu ya Madaraka nchini Kenya?

3. Taja sherehe za kitaifa zinazisherehekewa Kenya zilizotajwa kwenye shairi.

4. ___________________________________ ni siku kuu ya kitaifa inayofanyika kila Desemba tarehe kumi na mbili.

5. Mei mosi ni siku ya ________________________________

## ANAYEIPENDA NCHI

**Mtunzi : Ali M. Mwanza**
**Lakabu: Malenga Kande**
**Gatuzi: Kwale, Kenya.**

Wakenya tuamkeni, kupeperusha bendera,
Tupandize kileleni, wakenya siyo hasara,
Anayeipenda nchi, aiheshimu bendera.

Rangi nyeupe I ndani, ni rangi inopendeza,
Ndiyo rangi ya amani, rangi isiyochukiza,
Anayeipenda nchi, si kisasi kulipiza.

Tusiingie vitani, wengine kusukumana,
Kisha kuwachukiana, mkakosa kuonana,
Anayeipenda nchi, wengine kusemezana.

Wimbo nao heshimuni, kwani ndo wetu umoja,
Kiimba tuwe makini, ombi letu kwa pamoja,
Anayeipenda nchi, wimbo tuimbe pamoja.

Kisha kwenda shereheni, na wengine kuwaasa,
Sherehe za taifani, hizi ndo zangu hamasa,
Anayeipenda nchi, aende bila kukosa.

**Jitathmini**

1. Ni rangi gani ambayo huashiria amani kwenye bendera ya Kenya?

2. Tunaambiwa kama wakenya tuamke tu______________________________________________________________________________

3. Kichwa cha shairi hili ni ______________________________________________________________

4. Kamilisha sentensi hii

   Anayeipenda ____________________________________________ bendera.

5. Ni kitu gani ambacho tunatakikana kukiheshimu kwa sababu ni umoja wetu?

## NIDHAMU MEZANI

**Mtunzi : Ali M. Mwanza**
**Lakabu: Malenga Kande**
**Gatuzi: Kwale, Kenya.**

Mie mlo ninasema, ninapofika mezani,
Kinila wacha kusema, nisirudi sahanini,
Usiwe kama watema, napongia mdomoni,
Si nidhamu ninasema, kinila kuwa makini,
Kisonekane cha chuma, kilo kule kilimini,
Nitafune kiwa kimya, la kwanza hili fumbata.

Polepole nitafuna, kuniingiza tumboni,
Kisha unile kisena, kwamba tu sote keshoni,
Siwe tumbo kujazana, tumbo kawa taabani,
Kiisha tutaonana, tarudi tena mezani,
Cha kutosha kinafana, muhimu mwako mwilini,
Kinila usinijaze, muhimu hili chukuwa.

Wenzako wakiwa mbali, jipakulie makini,
Zijali na zao hali, kitangulia mezani,
Labuda yao ni kali, njaa inowakulani,
Daima lipinge hili, liwalo jambo la shani,
Sione uwapo wali, kachekea nafusini,
Ongeza wakitosheka, ndiyo staha mezani.

Kunila umesimama, si adabu sikiani,

Unile ukiwa wima, puani tapitiani,
Takuwacha ukihema, hewa nikikufungani,
Ubaki ukilalama, au hata kiliani,
Siende mezani wima, uwe nalo akilini,
Kunila umesimama, si adhabu ya mezani.

Chukua cha mbele yako, unapoweza fikani,
Kifanye halali yako, kwamba aali tumboni,
Vilo mbele ya wenzako, uwache kurukiani,
Iwache mirukoruko, kotekote wamenyani,
Siwe kama mbwakoko, wenzako kawaudhini,
Sivivute na kuomba, vya wengine kupapia.

Usile bila kunawa, unapofika mezani,
Mikono yako kinawa, tapata ua viini,
Maradhini kutengawa, nao wendani mezani,
Ukitimiza pakuwa, ili ulambe vyandani,
Upate tamu haluwa, ulofichika mloni,
Kimaliza pia nawa, ndiyo nidhamu mezani.

Uweke na Mola kwanza, unapongia mezani,
Kabula kula kuanza, kumshukuru manani,
Ni heshima kujifunza, ya Mungu kuruzukuni,
Hata kula kuwe panza, omba kifika mwishoni,
Vikusanye vyombo kwanza, na mabaki hifadhini,
Nakuasa zingatia, zote adabu mezani.

**Jitathmini**

1. Neno lipi linaweza kutumika badala ya adabu?
2. Shairi hili ni la aina gani? Kwa nini?
3. Taja adabu zozote 4 za mezani ulizojifunza kwenye shairi.
4. Unaponawa mikono ______________________________________________
5. Mshororo wa mwisho wa kila ubeti wa shairi hili huitwaje?
6. Kwa nini tunatakikana tule chakula cha kutosha?
7. Ni wakati gani tunapaswa kuongeza chakula kulingana na adabu mezani?
8. Kwa maoni yako, kwa nini mshairi ametumia vina vya mwisho vinavyofanana?
9. Wakaririe ndugu zako nyumbani shairi hili kwa mahadhi yanayopendeza.

## UZALENDO

**Mtunzi: Kipkoech Kelvin**
**Lakabu: Ustadh Salim**
**Gatuzi: Bomet, Kenya.**

Nasimama jukwaani, wakenya tumakinike,
Malenga wa kijijini, apendaye nchi yake,
Nisikizeni  makini, machache yangu yashike,
Wananchi wazalendo, tupiganie amani.

Sote tuwe wazalendo, tupende nchi kwa dhati,
Raia wenye upendo, wala sio wasaliti,
Pamoja kwenye mawindo, si siri kuna bahati,
Wananchi wazalendo, tupiganie amani.

Lije litakalokuja, liwe litakalokuwa,
Tukiungana pamoja, basi tutafanikiwa,
Tutapaa si hoja, tena mbali kama njiwa,
Wananchi wazalendo, tupiganie amani.

Amani tena amani, nasisitiza amani,
Ni kitu bora jamani, zawadi yenye thamani,
Taifa lenye amani, limeshika usukani,
Wananchi wazalendo, tipiganie amani.

Kikomo hapa natia, mnyonge naenda zangu,
Nilotunga metoshea, mengine nachia Mungu,
Amani nawaombea, awe nanyi baba Mungu,
Wananchi wazalendo, tupiganie amani.

**Jitathmini**

1. Lipe anwani mwafaka shairi hili
2. Eleza vina vya kati na mwisho katika ubeti wa pili
3. Eleza ujumbe unaojitokeza katika ubeti wa tatu
4. Mtunzi wa shairi hili anasisitiza nini
5. Eleza maana ya maneno haya

a) Jukwaani
b) Uzalendo
c) Amani
d) Thamani
e) Usukani

## NITAJIJUA

**Mtunzi: Geoffrey N. Ogola**
**Lakabu: Malenga Msanii**
**Gatuzi: Kakamega, Kenya.**

Salamu ni za shuleni, shule ni ya msingi,
Bagi yangu mgongoni, naenda kujua mengi,
Nikifika shulenini, nitajua mambo mengi,
Mtaala sasa mpya, tajijua kitalanta.

Nitaketi darasani, niyasome mambo mengi,
Kutoka viadani, niwe na akili nyingi,
Taweka daftarini, takayopata kwa wingi,
Mtaala sasa mpya, tajijua kitalanta.

Wazazi kule nyumbani, wamiliki furaha nyingi,
Mtoto wao shuleni, talanta kwenye kichungi,
Kujua nitafanyani, tafanyani na siringi?
Mtaala sasa mpya, tajijua kitalanta.

Wakiniona nyimboni, tunzi tanipa shilingi,
Wakiniona nyayani, handisi meme kiwingi,
Wakiniona dongoni, ufinyanzi ndiyo mwingi,
Mtaala sasa mpya, tajijua kitalanta.

Nicheze nyundo kononi, seremala mara nyingi,
Nikijipenda nyanjani, michezo kwangu kwa wingi,
Niwe mwenye unadini, dalali ndo yangu mingi,
Mtaala sasa mpya, tajijua kitalanta.

Nikipatwa ucheshini, uigizaji ndo mwingi,
Tajijua talantani, nitayafanya kwa wingi,
Hata niwe tarikini, nitahusika kiwingi,
Mtaala sasa mpya, tajijua kitalanta.

Kuna mengi asilani, sijayataja ni mengi,
Nafurahia shuleni, ninayopenda ndo mengi,
Hapa mie tamatini, nitarudi nayo mengi,
Mtaala sasa mpya, tajijua kitalanta.

Jitathmini

1. Shairi ili ni la aina gani?
2. Andika kibwagizo cha shairi hili.
3. Kwa nini mtunzi anafurahia shuleni?
4. Taja baadhi ya talanta kutoka shairini
5. Nani hutumia nyundo kazini?

## SALAMU

**Mtunzi: Timothy Omusikoyo Sumba**
**Lakabu: Malenga Mstaarabu**
**Gatuzi: Kakamega, Kenya.**

Sabalkheri naamba, akheri natarajia,
Kumekucha nenda shamba, salamu mekupatia,
Nipande hata mipamba, mikorosho na dania,
Asubuhi kumekucha, siache kunisalimu.

Masalkheri nakili, akheri wanijibia,
Jioni jua si kali, hali shwari naridhia,
Mbuzi kondoo fahali, zizini wakaingia,
Jioni inapotimu, siache kunisalimu.

Buriani e mwandani, mazuri nakutakia,
Tutaonana mwakani, kwa kudura za Jalia,
Nagura nenda mjini, nipate kujichumia,
Ninahama kijijini, siache kunisalimu.

Shikamoo wangu babu, marahaba wajibia,
Mengi yaliyonisibu, wewe linitatulia,
Ikanitoka aibu, aushi nafurahia,
Nikikuzuru kayani, siachi kukusalimu.

Makiwa ni kwetu sisi, tunayo twajililia,
Amefariki m'basi, macho amejifumbia,
Ni kweli sio tetesi, kaburi ataingia,
Huzuni imetufika, siache kutusalimu.

Habari yako mwandani, ni njema natarajia,
Nakutakia amani, kwako pia familia,
Tudumishe ujirani, zogo lisije tulia,
Muhimu ni utangamano, siache kunisalimu.

## TULENI VYAKULA BORA

**Mtunzi: Timothy Omusikoyo Sumba**
**Lakabu: Malenga Mstaarabu**
**Gatuzi: Kakamega, Kenya.**

Tuleni vyakula bora, miili ipate simama,
Tule maembe mapera, afya izidi tuama,
Na tufanyeni papara, tuleni tena kwa wima,
Tuleni vyakula bora, tuijenge mili yetu.

Zabibu pia na embe, tule tupate tofuma,
Tusiufanye uzembe, afya bora itahama,
Samaki haoti pembe, tule mboga nazo nyama,
Tuleni vyakula bora, tuijenge mili yetu.

Tuleni pia uanga, mwili siwe lele mama,
Mbogamboga za kutwanga, mahindi nawo mtama,
Si ndizi si kungu manga, tuleni tuwe salama,
Tuleni vyakula bora, tuijenge mili yetu.

Tuleni vya protini, misuli iwe 'ja chuma,
Tuvijaze matumboni, simba apate nguruma,
Tuleni vya vitamini,  zipungue kwetu homa,
Tuleni vyakula bora, tuijenge mili yetu.

Na tuyaleni mayai, kwa kasi bila huruma,
Tuyaacheni malai, mafuta yanasimama,
Barafu kwetu adui, tuache sio salama,
Tuleni vyakula bora, tuijenge mili yetu.

**Jitathmini**

1. Je, silabi ya shairi huitwaje?
2. Mstari mmoja wa shairi huitwaje?
4. Andika kibwagizo cha shairi hili.
5. Taja vyakula ambavyo si salama.

# MIEZI

**Mtunzi: Masika Derrick**
**Lakabu: Dokta Ziro**
**Gatuzi: Kakamega, Kenya.**

Mwezi wa kwanza ni Januari ,
Wa pili ni Februari ,
Wa tatu huwa ni Machi ,
Na wa nne Aprili .

Mwezi wa tano huwa Mei ,
Wa sita huwa ni Juni ,
Wa saba nao Julai ,
Na wa nane nane ni Agosti .

Mwezi wa tisa Septemba ,
Wa Kumi ni Oktoba ,
Kumi na moja ni Novemba ,
Kumi na mbili ni Desemba .

**Jitathmini**

1. Mwezi wa kwanza huitwaje ?
2. Mwezi wa tatu huitwaje ?
3. Agosti huwa mwezi gani ?

4 . Mwaka una miezi mingapi ?

5 . Mwezi upi huja kabla ya Julai ?

## PAKA WANGU

**Mtunzi: Masika Derrick**
**Lakabu: Dokta Ziro**
**Gatuzi: Kakamega, Kenya.**

Paka wangu ni mzuri,
Yeye hushika panya,
Panya naye analia,
Uuuuwi unaniua.

Anapenda kunywa maziwa,
Na pia kuota moto,
Hujilaza kwenye kochi,
Wakati amechoka.

Paka wangu ni mweupe,
Mweupe kama pamba,
Macho yake hupendeza,
Macho yake ni mazuri.

Paka wangu ana mbio,
Anapenda pia  kucheza,
Kucheza na vinyau,
Nampenda paka wangu.

**Jitathmini**

1. Paka hushika nini?
2. Paka anapenda kunywa nini?
3. Paka ni mweupe kama nini?
4. Paka anapenda kucheza na nani?
5. Paka hujilaza wapi akichoka?

## KAZI ZETU

**Mtunzi: Benson Baya Sulubu**
**Lakabu: Kaka Benaya (Malenga wa baharini)**
**Gatuzi: Kilifi, Kenya.**

Zipo kazi nyingi sana, tena nzuri kazi njema,
Kila siku twaziona, leo sasa twazisoma,
Tuzijue kwa mapana, tutambue kazi vyema,
Hizi ndizo kazi zetu, inafaa tuzijue.

Dakitari ni wa kwanza, huyu sote hututibu,
Wagonjwa anawatunza, huitwa pia tabibu,
Afya bora hutufunza, mili tusiiharibu,
Hizi ndizo kazi zetu, inafaa tuzijue.

Twende sasa kwa mwalimu, huyu mtu ni muhimu,
Nyote munamufahamu, hutupa sisi elimu,
Hufundisha humu humu, sote tunamuheshimu,
Hizi ndizo kazi zetu, inafaa tuzijue.

Tumjue mkulima, hufanya kazi shambani,
Kazi yake ni kulima, tumfahamu jamani,
Mpishi tutamsema, hutupikia jikoni,
Hizi ndizo kazi zetu, inafaa tuzijue.

Seremala wa samani, huunda vitu vya mbao,
Tusimwache na mshoni, anatushonea nguo,
Tuwajue marubani, hupaa na ndege zao,
Hizi ndizo kazi zetu, inafaa tuzijue.

Dereva huwa wa gari, mfinyanzi wa udongo,
Bawabu ni askari, husimama kwenye lango,
Tuzijue vizuri, mwashi fundi wa majengo,
Hizi ndizo kazi zetu, inafaa tuzijue.

Kinyozi hunyoa nywele, mrina ni wa asali,
Kweli kazi ziko tele, manahodha ni wa meli,
Msusi husuka nywele, sheria ni ya wakili,
Kweli kazi ziko nyingi, hizi haziishi leo.

**Jitathmini**

1. Daktari hufanya kazi gani?
2. Daktari pia huitwa nani?
3. Nani hufanya kazi ya kufundisha?
4. Mkulima hufanya kazi gani?
5. Mpishi hupikia wapi?
6. Seremala hufanya kazi gani?
7. Anayeshona nguo anaitwaje?
8. Dereva anafanya kazi gani?

9. Eleza kazi mbili zilizotajwa katika ubeti wa mwisho.

## NAOMBA HAKI

**Mtunzi: Benson Baya Sulubu**
**Lakabu: Kaka Benaya (Malenga wa baharini)**
**Gatuzi: Kilifi, Kenya.**

Najizua haki zangu, sasa nazifahamu,
Elimu ni haki yangu, ni haki yangu muhimu,
Nikikosa ni uchungu, huona kama hukumu,
Nipewe haki zangu, tafadhali ninaomba.

Nipatiwe lishe bora, afya yangu iwe nzuri,
Niishi maisha bora, maisha yangu mazuri,
Nifurahi kila mara, nikiona haki nzuri,
Nipewe haki zangu, tafadhali ninaomba.

Nipewe pia mavazi, nipendeze kwa wenzangu,
Ninawaomba wazazi, msikie ombi langu,
Nisionekane chizi, mavazi ni haki yangu,
Nipewe haki zangu, tafadhali ninaomba.

Matibabu nisikose, najua pia ni haki,
Naogopa mnitese, hilo mimi silitaki,

Mimi musininyanyase, hiyo si haki yangu,
Nipewe haki zangu, tafadhali ninaomba.

Iwapo nitaugua, dakitari anione,
Aweze kunikagua, ili ugonjwa upone,
Msiseme nasumbua, ni haki zipatikane,
Mimi mtoto jamani, nazijua haki zangu.

**Jitathmini**

1. Haki gani mwandishi akikosa huhisi uchungu?
2. Nini humfanya anayezungumza kufurahi kila mara?
3. Iwapo ataugua nani anafaa kumwona?
4. Ni nini si haki yake anayezungumza?
5. Taja sababu tatu kwa nini haki ni muhimu.

## VYAKULA VYA MADHARA

**Mtunzi: Isaac Kisa Juma**
**Lakabu: Malenga wa Kanisani**
**Gatuzi: Kakamega.**

Lishe bora ni muhimu,
Kwetu sisi binadamu,
Afya njema hutukimu,
Ndiposa twatabasamu.

Vyakula vyote si bora,
Ila twala kwa papara,
Hatuli vilivyo bora,
Mwisho vyaleta madhara.

Chumvi naanza kusema,
Kiasi tuweze pima,
Tumbo zisije kuuma,
Wala tuanze kuhema.

Huwa ni tamu sukari,
Ila tena ni hatari,
Magonjwa huyasitiri,
Kama vile kisukari.

Soda nayo ni kinywaji,
Kinao wengi wanywaji,

Wanywa bila kuhoji,
Matokeo ya unywaji.

Hula nazo bisikuti,
Na tena kila wakati,
Wala hata kwa umati,
Na miswaki hawapati.

Peremende watafuna,
Midomoni utaona,
Mashavuni waguguna,
Wengi huwa ni vijana.

Sharubati wabugia,
Na kunywa kama ngamia,
Magonjwa wajijazia,
Tumboni yawaingia.

Vibanzi navyo sikia,
Njiani wakaangia,
Huku vumbi lafukia,
Tusile kwa kubugia.

Huwa tamu chokoleti,
Humumunywa kama switi,
Huwthiri kwa wakati,
Meno 'kiingia kati.

**Jitathmini**

1. Mwandishi anasema kuwa vyakula vyote si bora. Kwa nini?
2. Kwa nini tunaonywa kuhusu matumizi ya sukari nyingi?
3. Mshororo wa kwanza una mizani mingapi?
4. Chokoleti imefananishwa na switi kwa njia gani?
5. Peremende huliwa sana na watu wa Aina gani?

## VYAKULA BORA

**Mtunzi: Isaac Kisa Juma**
**Lakabu: Malenga wa Kanisani**
**Gatuzi: Kakamega.**

Tunavyo vyakula bora,
Visivyoleta madhara,
Tuvile mara kwa mara,
Hivyo hung'arisha sura.

Yatunde mengi matunda,
Yale unayoyapenda,
Miembe mipera panda,
Uani yaweze Wanda.

Kwa wingi ramba asali,
Hutupa ladha asili,
Sukari yake halali,
Ya kuipa kinga mwili.

Ndizi ukila kwa wali,
Na sukuma kwa ugali,
Ndivyo vyakula halali,
Tumboni tuvisajili.

Madondo kwayo chapati,

Kanza katu hatupati,
Umefanywa utafiti,
Na kuwekwa kwa gazeti.

Viazi haswa vitamu,
Madini mengi hukimu,
Mwili huongeza damu,
Kwayo tuzidishe hamu.

Tuile nyeupe nyama,
Pamoja nayo sukuma,
Epuka nyekundu yama,
Hiyo kwetu si salama.

Mayai tule kadiri,
Mengi huwa ni hatari,
Kwa kunde tuyasitiri,
Iwe ni yetu desturi.

Magonjwa tutadhibiti,
Sote tukijizatiti,
Tufwate haya masharti,
Hapa nafika tamati.

**Jitathmini**

1. Shairi hili linazungumzia Nini?
2. Kwa nini tunaambiwa turambe asali kwa wingi?
3. Shairi hili lina beti ngapi?
4. Je, ni salama kula nyama nyekundu?

5. Vyakula bora ni vipi?

## VYAKULA HATARI

**Mtunzi: Faith Machayo**
**Lakabu: Malenga mjini**
**Gatuzi: Trans Nzoia, Kenya.**

Sisi wadogo watoto,
Tunapenda biskuti,
Tunapenda pia loto,
Sisahau chokoleti,
Mwilini vyaleta joto,
Sababu ya sharubati,
Tudumishe lishe bora
Tusishikwe na maradhi.

Chipsi chipsi kuku,
Ni tamu kama halua,
Tunaila kila siku,
Mandara yametujua,
Nakashifu si udaku,
Chipsi itatuua,
Tudumishe lishe bora,
Tusishikwe na maradhi.

Sherehe za kuzaliwa,

Nani asiyeipenda?
Kakeki tunakatiwa,
Maana tunakapenda,
Madhara yake simuliwa,
Hakika hautapenda,
Tudumishe lishe bora,
Tusishikwe na maradhi.

Wapenzi nawaeleza,
Lishe bora ni muhimu,
Maradhi yatatusaza,
Tukiila pia msimu,
Tusije tukateleza,
Na chakula vili simu,
Tudumishe lishe bora,
Tusishikwe na maradhi.

**Jitathmini**

1. shairi hili lina beti ngapi?
2. Andika kibwagizo cha shairi hili.
3. Shairi hili linasema kuwa watoto wanapenda nini?
4. Chipsi kuku ni tamu kama nini?
5. Keki huliwa wakati upi?

## KARIBU DARASANI

**Mtunzi: Erick Teitei Muteti**
**Lakabu: Malenga Chaja ya Kobe**
**Gatuzi:**

Karibuni darasani, daraja yetu ya kwanza,
Keti mwana dawatini, ubao kitu cha kwanza,
Chaki ni ya ubaoni, chaki kalamu ya mwalimu,
Karibuni darasani, gredi ni ya kwanza.

Darasani pana kitabu, mambo bora tusomeni,
Madaftari na vitabu, yote yapo kabatini,
Hati bora kwa kitabu, kora bora vitabuni
Karibuni darasani, gredi ni ya kwanza.

Ticha nipe kichongeo, nichonge kalamu yangu,
Peni ‘taka kichongeo, uipende hati yangu,
kichongapo kichongeo, utaipenda hati yangu,
Karibuni darasani, gredi ni ya kwanza.

Usiile raba Kozi, raba chafu si bora,
Usifutefute kazi, matini chafu si bora,

Kwa makini futa kazi, usafi kazini bora,
Karibuni darasani, gredi ni ya kwanza.

**Jitathmini**

1. Ukiwa na rafiki yako ,taja vifaa vitatu vya darasani kwenye shairi.

_________________

_________________

_______________

2. Wasamabzie wanafunzi wenzako na marafiki shairi hii mtandaoni ili waisome?

## MIEZI YA MWAKA

**Mtunzi: Zacky Nebar**
**Lakabu: Malenga Mhanguzi**
**Gatuzi: Laikipia, Kenya.**

Januari ndiyo mosi, kwenye kalenda ya mwaka,
Hapa ndipo kiongozi, hufanya yote kauka,
Februari kwa kasi, kwa siku chache hakika.
Nakufunza msomi, jua miezi ya mwaka.

Mwezi Machi hufuata, kiangazi huzamishwa,
Mvua nayo hukita, ni mengi sana huoshwa,
Aprili huwa ngota, na wasafiri hutishwa,
Nakufunza msomi, jua miezi ya mwaka.

Mei ni mwezi wa tano, Juni hufuata mbele,
Mvua hupua mno, mwanzo wa baridi tele,
Julai ndiyo hino, watu hufunika nywele.
Nakufunza msomi, jua miezi ya mwaka.

Agosti ni ya nane, Septemba huja tisa,
Hatupati hata tone, mazao huja kutesa.
Hubidi watu ungane, kuvuna pasi kukosa,
Nakufunza msomi, jua miezi ya mwaka.

Oktoba huja kumi, yakufuata Novemba,
Disemba hujakukomi, ndiyo mwisho wa kasumba,
Naichana mbuga mimi, nimekupa yalobomba,
Nakufunza msomi, jua miezi ya mwaka.

## NG'OMBE WETU

**Mtunzi: Agadias Ikoha**
**Lakabu: Malenga wa Nyali One**
**Gatuzi: Mombasa, Kenya.**

Ng'ombe wetu ni mkubwa, anazo pembe kichwani,
Kama nyati kiukubwa, wanafanana usoni,
Ng'ombe ana nundu kubwa, iliyoko mgongoni,
Ng'ombe wetu twampenda.

Ng'ombe hulala zizini, usiku unapofika,
Hupelekwa malishoni, naye baba ama kaka,
Hufungwa kamba shingoni, asije akatoroka,
Ng'ombe wetu twampenda.
Mwana wa ng'ombe ni ndama, yeye hukimbia sana,
Ng'ombe hutengwa na ndama, huzuiwa kwandamana,
Ng'ombe wetu huroroma, na wengine kikutana,
Ng'ombe wetu twampenda.

**Jitathmini**

1. Mwana wa ng'ombe huitwaje?
2. Mbona ng'ombe hufungwa kamba shingoni?
3. Pembe za ng'ombe huwa katika sehemu ipi ya mwili?
4. Mgongoni ng'ombe huyu ana nini?

5. Ng'ombe hulala wapi?

## HAKI ZETU

**Mtunzi: Agadias Ikoha**
**Lakabu: Malenga wa Nyali One.**
**Gatuzi: Mombasa, Kenya.**

Mama naomba sikiza,
Haki zetu nakujuza,
Sitaki kuzipoteza.
Tunahitaji elimu,
Maishani ni muhimu,
Tukisoma tajikimu.
Amesema mtulinde,
Vilevile mtupende,
Nasi pia tuwapende.
Mtupatie mavazi,
Pamoja nayo malezi,
Majukumu ya wazazi.
Sisahau bora lishe,
Hilo mama usibishe,
Magonjwa ituepushe.

**Jitathmini**

1. Taja faida ya elimu?
2. Ni nani anafaa kulindwa na kupendwa?

3. Ni jukumu la nani kumpa mtoto malezi?
4. Tukipata lishe tutaepuka kupata nini?

## SIKU YA SOKO

**Mtunzi: Erick Omondi**
**Lakabu: Babu Mesh**
**Gatuzi: Siaya, Kenya.**

Asubuhi na mapema, hatukuenda shuleni,
Nilikuwa naye mama, tulipoenda sokoni,
Wala hatukusimama, kikapu nacho begani.

Tulipitia dukani, bila kukuwa na pupa,
Tulinunua majani, mama yangu akalipa,
Tukaongeza sabuni, maziwa pia kukopa.

Nyama pia kwa mizani, na sukari kwa ratili,
Mama akalipa deni, akamaliza bili,
Kafika mkokoteni, na mbele yake hamali.

Wateja walijazana, wakitaka kununua,
Wauzaji kupishana, bei wakiziamua,
Nilifurahia sana, nyumbani tukirejea.

## SIKU YA SOKO

### Jitathmini

1. Kikapu hutumiwa kufanya nini?
2. Tunaponunua bidhaa huwa tunalipa kutumia nini?
3. Hamali hufanya kazi gani?
4. Siku yenu ya soko ni lini?
5. Je, ushawahi kutumwa sokoni? Ulitumwa nini?

## USAFI WA MWILI

**Mtunzi: Sophie Binsari**
**Lakabu: Trabizuna ya Jangwani**
**Gatuzi: Kisii, Kenya.**

Usafi jambo  muhimu, sote tuuzingatie,
Kuoga iwe jukumu, kamwe tusipuuzie,
Miili safi muhimu, siku zote tuwe safi.

Nywele zako uzichane, kichana usikose,
Kucha nazo ukazane, zikikua zipunguse,
Miili safi muhimu, siku zote tuwe safi.

Yasugue yako meno, kila baada ya kula,
Uoshe nayo mikono, unapotoka msala,
Miili safi muhimu, siku zote tuwe safi.

Nguo zako zisafishe, kwa maji nayo sabuni,
Daima jinadhifishe, nyumbani hata shuleni,
Miili safi muhimu, siku zote tuwe safi.

**Jitathmini**

1. Shairi hili lina beti ngapi?
2. Meno husafishwaje?

3. Kibwagizo cha shairi hili ni...
4. Kwa nini ni muhimu kunawa
5. Eleza ujumbe wa shairi hili

## FAMILIA YETU

**Mtunzi: Robert Bin Kirui**
**Lakabu: Malenga Chumamoto**
**Gatuzi: Nandi, Kenya.**

Jina langu ni Katana,
Ninasoma Majangina,
Mwalimu wangu ni Sena,
Ninampenda daima,

Baba yangu ni Faulu,
Mama yangu ni Kalulu,
Shangazi pia ni Telu,
Ninawapenda daima.

Kaka yangu ni Mwema,
Dada yangu ni Fatuma,
Wao husoma Salama,
Ninawapenda daima.

Rafiki yangu ni Chumba,
Tunayo miaka saba,
Kwao kwetu mkuruba,
Ninampenda daima.

Mtaa wetu ni Dimba,
Dimba kuna akraba,
Kiongozi wetu - Mamba,
Ninampenda daima.

MASWALI:

1. Mistari katika ubeti huitwaje?
2. Kila ubeti wa shairi hili una mishororo mingapi?
3. Shairi hili lina kipande kimoja, kitaje.
4. Mshororo wa kwanza, ubeti wa watu una mizani mingapi?
5. Shairi hili linatoa ujumbe upi?

## KAZI MBALIMBALI

**Mtunzi: Robert Bin Kirui**
**Lakabu: Malenga Chumamoto**
**Gatuzi: Nandi, Kenya.**

Nikiwa mkubwa
Walimu tufunzeni, shuleni sasa twasoma,
Mwishowe niwe rubani, ama sogora wa ngoma,
Mwenzangu awe mshoni, muuguzi si mgema,
Ewe Mungu nijalie, mustakabali heri.

Ama niwe wakili, haki kuzipatikana,
Nisiwe kuli,hamali, bawabu wala mrina,
Nahodha nendeshe meli, rafiki awe gavana,
Ewe Mungu nijalie, mustakabali heri.

Kaka awe daktari, dada awe kandawala,
Ama hata askari, mwashi pia seremala,
Siwe utingo wa gari, heri dereva wa trela,
Ewe Mungu nijalie, mustakabali heri.

Mwenzangu uwe karani, hadhari kuwa mkwezi,
Au msusi saluni, mfinyanzi na kinyozi,
Umaskini si fani, afadhali muunguzi,

Ewe Mungu nijalie, mustakabali heri.

Kazi niweze kufanya, ni matunda ya elimu,
Wazazi na wanionya, nithamini binadamu,
Heshima pia kumanya, niwe mwema mhudumu,
Ewe Mungu nijalie, mustakabali heri.

## KORONA LITOKA WAPI?

**Mtunzi: Christopher Musa Kalunda**
**Lakabu: Malenga Mwepesi**
**Gatuzi: Vihiga**

Wazazi wetu nyumbani, sisi nasi skulini,
Popote pale wandani, ugonjwa huu shetani,
Tumwombe wetu Manani, atulinde duniani,
Mwenzenu ninauliza, korona litoka wapi?

Barakoa tumevaa, mikono twajinawia,
Usafi twazingatia, sheria twafwatilia,
Serikali nayo pia, sikio twawapatia,
Mwenzenu ninauliza, korona litoka wapi?

Walimu nao shuleni, ugonjwa mewatishia,
Madaktari jamani, pia nao mehofia,
Dawa zote wandani, kwa korona zaishia,
Mwenzenu ninauliza, korona litoka wapi?

Maisha tunayajali, usiku nao mchana,
Tukimuomba Jalali, bayana tukipambana,
Sote kwa hali na mali, tunajikinga korona,
Mwenzenu ninauliza, korona litoka wapi?

Sasa mzaha hakuna, masomo tuliyakosa,
Waja liwaua sana, wengine wakiwa sasa,
Wavyele kazi hawana, hela pia wakakosa,
Mwenzenu ninauliza, korona litoka wapi?

Kaditama natimia, na wangu huu wosia,
Ni bora kuzingatia, afya bora na sheria,
Siku moja tatimia, korona tatwondokea,
Mwenzenu ninauliza, korona litoka wapi?

**Jitathmini**

1. Shairi hili lina beti ngapi?
2. Mshororo wa mwisho unaorudiwarudiwa katika kila ubeti unaitwaje?
3. Mwandishi ana ujumbe upi katika aya ya mwisho?
4. Taja vina vya ndani na nje vya ubeti wa kwanza.
5. Taja kibwagizo cha shairi hili.
6. Nini maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumika katika shairi.
    a). Wakiwa
    b). Korona
    c). barakoa

## VIKEMBE

**Mtunzi: Christopher Musa Kalunda**
**Lakabu: Malenga Mwepesi**
**Gatuzi: Vihiga**

Chukua kalamu sasa, tusome vikembe vyetu,
Sote kwetu yatupasa, tusikanganyike katu,
Tuvitaje bila kosa, tuwafae na wenzetu,
Ni vitoto vya viumbe, tujuwe vyetu vikembe.

Mwanadamu ana mwana, cha tembo kite kidanga,
Kitoto cha nyuki, jana,cha kuku ni kifaranga,
Na mamba ana kigwena, kitoto chake kichanga,
Ni vitoto vya viumbe, tujuwe vyetu vikembe.

Kinyemere ni cha nyoka, hutototolewa kwa yai,
Kinyaunyau cha paka, na chui ana kisui,
Kwa mbuzi naye kisaka, hutamkosa kibui,
Ni vitoto vya viumbe, tujuwe vyetu vikembe.

Kipuku sije sahau, ni kitoto chake panya,
Na nyangumi ni falau, kukijua kinyangunya,
Na shibli sidharau, simba akakutapanya,
Ni vitoto vya viumbe, tujuwe vyetu vikembe.

Napo kiotani nyuni, vijue vyake makinda,
Na kihongwe wa nyumbani, ni kitoto chake punda,
Nyumbu pia fahamuni, ni cha farasi na punda,
Ni vitoto vya viumbe, tujuwe vyetu vikembe.

Nyumbani tuna vipura, ni vitoto vyake njiwa,
Viluwiluwi vya chura, mbweha ana nyamawa,
Kikangazi yake sura, na mamaye tai sawa,
Ni vitoto vya viumbe, tujuwe vyetu vikembe.

Kondoo ana kitoto, kinachoitwa katama,
Bakaya au kikuto, humuita fisi mama,
Kiboko katika mto, kigubu huwa salama,
Ni vitoto vya viumbe, tujuwe vyetu vikembe.

Somo kituo natia, ni vingi sitamaliza,
Kuvilinda ni sheria, na salama kuvikuza,
Vizazi vikendelea, Moliwa akatutuza,
Ni vitoto vya viumbe, tujuwe vyetu vikembe.

**Jitathmini**

1. Shairi hili linazungumzia nini?
2. Kibwagizo katika shairi hili ni kipi?
3. Mtunzi stadi wa mashairi na nyimbo anaitwaje?

4. Mtoto wa fisi anaitwaje?
5. Shairi hili linatufunza nini?

## MAMA YANGU

**Mtunzi: Stephen Oluoch**
**Lakabu: Malenga Anzalisteve**
**<u>Gatuzi: Migori</u>**

Nakupenda mama yangu, hakuna akushindiye
Kukulinda kazi yangu, amani nikupatiye
Nitumia mali yangu, maisha ufurahiye
Mama Jeni mama yangu, pokea heshima zako

Kati ya watu muhimu, nakuweka namba wani
Naomba mungu udumu, unifae maishani
Kwa nyimbo zako matamu, uniondoe huzuni
Mama Jeni mama yangu, pokea heshima zako

Ulicheka nikicheka, beleko kunibebea
Hatarini kunishika, ulinzi hukulegea
Hata katika talaka, mama ulinitetea
Mama Jeni mama yangu, pokea heshima zako

Ulipitia machungu, nashindwa kuhesabia
Ukawa mwalimu wangu, lugha ukanifunzia
Nazungumza kizungu, mwanao nafurahia
Mama Jeni mama yangu, pokea heshima zako

Kalamu naweka chini, hapa natia kikomo
Nikafike kibandani, nifurahishe  mdomo
Chakula nitie ndani, nikarudie masomo
Mama Jeni mama yangu, pokea heshima zako

**Jitathmini**

1. Taja aina ya shairi hili
2. Kulingana na mshairi mama ana umuhimu gani katika jamii?
3. Taja sifa za mama kulingana na mshairi.
4. Mshairi anampangia nini mamake?
5. Chambua maudhui ya shairi hili.

## USAFI

**Mtunzi: Sharon Wekesa**
**Lakabu: Malkia wa Ushairi**
**Gatuzi: Trans Nzoia, Kenya.**

Naamka asubuhi, Maulana kumuomba,
Kisha bafuni nawahi, pasipo na kujigamba,
Mama alishanasihi, mazoea kujipamba,
Usafi kizingatia, na maisha tavutia.

Nitaoga uso wangu, miguu na hata mikono,
Nitaosha mwili wangu, kwa moyo uso msono,
Kwayo maji safi chungu, kiyateka kwa mikono,
Usafi kizingatia, na maisha tavutia.

Sifongo tanisugua, tena kwa yangu sabuni,
Mswaki n'taupigia, meno meupe jamani,
Tena nitasukutua, maji yafike pembeni,
Usafi kizingatia, na maisha tavutia.

Nguo safi tavalia, zile chafu nitaosha,
Hakika nitang'aria, malaika tanipisha,
Tena nitajivunia, hali yangu kuridhisha,
Usafi kizingatia, maisha tavutia.

Kucha ndefu nitakata, nazo nywele nitachana,
Najua nitakipata, kilicho changu kitana,
Kiooni sitasita, nitapendeza kwa sana,
Usafi kizingatia, maisha tavutia.

**Jitathmini**

1. Mtunzi anapoamka asubuhi, kitu cha kwanza anachofanya ni nini?
2. Kwa nini mtunzi anahimiza kuzingatia usafi?
3. Je, mtunzi atazichana nywele kwa kutumia nini?
4. Ili kuzifua nguo zing'are, unahitaji nini na nini?
5. Kulingana na ubeti wa mwisho, mtunzi atapendeza kama nani?

## MAPISHI

**Mtunzi: Sharon Wekesa**
**Lakabu: Malkia wa Ushairi**
**Gatuzi: Trans Nzoia, Kenya.**

Ni mpishi maridadi, nyanya yangu alo tuli,
Hupika kwa ustadi, vyakula vya kiasili,
Siku zote kashitadi, kwa bidii kila hali,
Kwa vyakula vya asili, muulize wangu nyanya.

Anaposiaga mtama, huchanganya na mawele,
Mahindi yale ya sima, hayaweki tele tele,
Hupika kwa kujinyima, uji mtamu u tele,
Kwa vyakula vya asili, muulize wangu nyanya.

Huchemsha na Viazi, vikuu tena vitamu,
Maboga hupika wazi, tukamumunya kwa hamu,
Tena kwenye lake vazi, anaposhika hatamu,
Kwa vyakula vya asili, muulize wangu nyanya.

Anapopika mlenda, mchicha na hata ndizi,
Jamani huwezi dinda, nakwambia waziwazi,
Utakula kwa mafunda, kwa huo wake ujuzi,
Kwa vyakula vya asili, muulize wangu nyanya.

**Jitathmini**

1. Mtunzi wa shairi hili anamsifia nani? Kwa nini?
2. Shairi hili lina beti ngapi?
3. Mtunzi ametaja vyakula vingapi katika shairi hili?
4. Je, nini maana ya " chakila cha kiasili"?
5. Je, unadhani kwa nini vyakula vya kiasili ni muhimu?

## HAKI YANGU

**Mtunzi: Sharon Wekesa**
**Lakabu: Malkia wa Ushairi**
**Gatuzi: Trans Nzoia, Kenya.**

Ninajua haki zangu, japokuwa ni mchanga,
Nitataja kwa mafungu, na heshima nitachunga,
Kwanza lishe bora yangu, isokuwa na majanga,
Haki yangu kitimiza, Mola akubarikiye.

Shule jama nipeleke, sitaki kuajiriwa,
Nataka nielimike, niwe wa kuheshimiwa,
Kwa ujenzi nihusike, na mfano kupigiwa,
Haki yangu kitimiza, Mola akubariye.

Nayahitaji malezi, yale yalo bora bora,
Tena nipawe mavazi, na kulindwa kila mara,
Nalo penzi la wazazi, linirushe ja tiara,
Haki yangu kitimiza, Mola akubarikiye.

Nacho kichwa kikiuma, matibabu niyapate,
Nisiteswe ja mnyama, na machozi nisifute,
Kisha nimwombe karima, baraka zikufuate,
Haki yangu kitimiza, Mola akubarikiye.

**Jitathmini**

1. Shairi hili lina beti ngapi?
2. Kulingana na shairi hili haki ya mtoto ni gani?
3. Anayetimiza haki za mtoto, atalipwaje kulingana na kifungu?
4. Mtoto anataka kupewa haki gani?
5. Kwa nini mtoto hataki kuajiriwa kulingana na ubeti wa pili?

## KAZI

**Mtunzi: Sharon Wekesa**
**Lakabu: Malkia wa Ushairi**
**Gatuzi: Trans Nzoia, Kenya.**

Mwalimu natua kwako, swali langu nalileta,
Mafunzo yenye mshiko, akilini yalinata,
Ila ninalo sumbuko, maini yakatakata,
Nichague kazi gani? Kwani zote nazienzi.

Napokuwa daktari, maisha nitaokoa,
Muuguzi si dosari, jamani tajivunia,
Na mkulima mahiri, waja nikiwalisha,
Nichague kazi gani? Kwani zote nazienzi.

Ama basi niwe mwashi, maghorofa niyajenge,
Namkumbuka mpishi, na michuzi niiunge,
Ninaipata tafashi, vipi nchi niijenge?
Nichague kazi gani? Kwani zote nazienzi.

Naona niwe wakili, wanyonge kuwatetea,
Sitaki kuwa hamali, uchovu kujiletea,
Ama rubani kwa hali, ndege nije itumia,
Nichague kazi gani? Kwani zote nazienzi.

Kaditama natimia, mwisho wangu nimefika,
Swali langu nawachia, li wazi laeleweka,
Mwalimu tanijibia, ili niwe na hakika,
Nichague kazi gani? Kwani zote nazienzi.

**Jathmini**

1.Shairi hili lina beti ngapi?

2. Je, kila ubeti una mishororo mingapi?

3. Katika ubeti wa tatu, mshororo wa pili, mtunzi anataka kuwa nani?

4. Je, mtunzi amewataja wafanyakazi wangapi katika shairi hili?

5. Mtunzi anaomba kusaidiwa kufanya nini?

## VYAKULA BORA

**Mtunzi: Victoria Wamwoyo**
**Lakabu: Bi. Victoria**
**Gatuzi: Kakamega, Kenya.**

Vyakulani salama, protini kuchaguliya,
Ya ng'ombe pia nyama, samaki nakutajiya,
Mimea protini njema, madondo hata ndengu.

Maziwa hata mayai, mwili wangu kuujenga,
Afya bora sikatai, kula vizuri ukichunga,
Protini nying haifai, unene utakufunga.

Wanga ni nguvu kucheza, ugali kuufinyanga,
Chapati nimeagiza, mihogo sijaifunga,
Viazitamu timiza, kwa uji sipate chenga.

Wanga vya kukupa nguvu, mkate tu asubuhi,
Wali chamcha tulivu, vyakula bora 'kusihi,
Mwili usiwe legevu, maji ni uhai sahihi.

Magonjwa kuyazuia, vitamini maradufu,
Mboga zote tafunia, matunda siwe pungufu,
Miwa na asali tumia, mwili kujenga nafuu.

## USAFI WA MAZINGIRA

**Mtunzi: Victoria Wamwoyo**
**Lakabu: Bi. Victoria**
**Gatuzi: Kakamega, Kenya.**

Mazingira niyatunze,
Ufagio nifungie,
Nyumba mara nifagie.

Reki kule nje nitumie,
Uchafu mwingi nibuyiye,
Kisha kwenye pipa.

Mazingira niyatunze,
Uchafu wote jaani,
Choo kiwe safi pia.

Nizuie kuendesha tumbo,
Nawa mikono kitoka msalani,
Usafi ni afya bora.

Miti niipande tena,
Hewa safi kuniletea,
Mazingira niyatunze.

## KALAMU IMEPOTEA

**Mtunzi: Erick Wasike**
**Lakabu:  Sumu ya Bafe**
**Gatuzi: Bungoma, Kenya.**

Nimefika jukwaani, sina furaha moyoni,
Nisikize kwa makini, nilipokuwa njiani,
Safari ya vichakani, shanta yangu mabegani,
Nimepoteza kalamu, naitafuta sipati.

Peke yangu njiani, kalamu anguka chini,
Mbiombio sikulini, pasi yangu maakini,
Kutazama mkopani, loh! Machozi mashavuni,
Nimepoteza kalamu, naitafuta sipati.

Nachomoka darasani, kuitafuta kalamu,
Nahemahema njiani, sababu yangu kalamu,
Mejitia matatani, ninaingoja hukumu,
Nimepoteza kalamu, naitafuta sipati.

Nimeanza kulialia, kutafuta nimechoka,
Wasiwasi meniingia, masomo yanafanyika,
Mwandani akanijia, wake moyo mepondeka,
Nimepoteza kalamu, naitafuta sipati.

Huruma kanifanyia, pamoja tukatafuta,
Muda haukukawia, kalamu tukaipata,
Sasa ninajivunia, wangu mwenzi kumpata,
Nimepoteza kalamu, naitafuta sipati.

Rafiki mtu muhimu, tuutunze urafiki,
Uliye naye mweshimu, epukana unafiki,
Pia nao ukarimu, mtunzane kwa haki,
Kalamu nimeipata, sasa ninafurahia.

## MWALIMU

**Mtunzi: Erick Wasike**
**Lakabu: Sumu ya Bafe**
**Gatuzi: Bungoma**

Shikamoo mualimu, pokea zetu salamu,
Wewe kwetu ni muhimu, unatufunza kwa hamu,
Twakuombea Rahimu, akupe nyingi fahamu,
Wewe johari adimu, hakuna alo mfano.

Mwalimu tunakupenda, penzi letu la dhati,
Wewe pia watupenda, na moyo wako wa dhati,
Kazi nayo waipanda, wafanya kwa utendeti,
Wewe johari adimu, hakuna alo mfano.

Elimu ya umilisi, mwalimu unatufunza,
Haufanyi kwa papasi, heshima unaitunza,
Wala hauendi kasi, kwa maakini wafunza,
Wewe johari adimu, hakuna alo mfano.

Polepole waeleza, twasikiza kimakini,
CBC yatupendeza, kama masomo nyanjani,
Mwalimu waelekeza, bila nyingi mtimani,
Wewe johari adimu, hakuna alo mfano.

Ahsante sana mwalimu, tunayo nyingi fahari,
Wanafunzi tuheshimu, mwalimu awe na heri,
Tuushike ukarimu, kila jambo liwe shwari,
Wewe johari adimu, hakuna alo mfano.